JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Dodoma
27 Novemba, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa viongozi mbalimbali. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka, viongozi walioteuliwa ni kama ifuatavyo:-

i. Prof. David Homeli Mwakyusa ameteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS);

ii. IGP Mstaafu Said Ally Mwema ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania (TSN). IGP Mstaafu Mwema anachukua nafasi ya Bw. Hab Mkwizu ambaye amemaliza muda wake; na

iii. Mhandisi Mussa Bally Natty ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB). Mhandisi Natty anachukua nafasi ya Bw. Joseph Odo Haule ambaye amemaliza muda wake.

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu